# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO –MKOA GEITA

Namba ya za simu
Mkuu wa shule 0753-452700
Makamu mkuu wa shule 0763-565968

SHULE YA SEKONADARI MAGUFULI
S . L . P – 7 6 > C H A T O.
Tarehe 12 / 06 / 2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..............................................................................................
S . L . P ..............................................................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAGUFULI HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO MKOA WA GEITA . MWAKA WA MASOMO 2023/2024 MCHEPUO WA ..................................**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (V) katika Shule ya Sekondari Magufuli kwa mwaka wa masomo **2023/2024**, katika mchepuo wa……....
Shule ya sekondari **Magufuli** ipo umbali wa kilometa **2** Magharibi mwa mji wa **Bwanga Wilaya ya Chato Mkoani Geita**.
Usafiri wa kutoka mjini unapatikana katika kituo cha Mabasi / Pikipiki - **Bwanga**.
Nauri ni shilingi **1,000/=** mpaka Shuleni.
Muhula wa masomo kwa kidato cha tano **(V) 2023/2024** utaanza tarehe **13/08/2023**
Hivyo Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe tajwa hapo juu bila ya kuchelewa.
Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023** si zaidi ya wiki mbili(2) toka Shule kufunguliwa.

## 1. MICHANGO MUHIMU YA SHULE:

**Michango inayotakiwa kulipwa na kila Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ni kama ifuatayo:**

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **JUMLA YA MICHANGO YOTE** | | **80,000/=** |

- **Fedha hizo zilipwe kupitia Benk ya NMB akaunti Na:- 32701200079**
- **Jina la akaunti – “Magufuli High School reccurent account”.**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2:1. Sare ya Shule:-

a) Shati nyeupe mbili(2) za mikono mirefu.
b) Suruali 2 rangi ya khaki, pia zinapatikana Shuleni
c) Suruali 2 nyeusi za kufanyia kazi za usafi na kushindia baada ya masomo.
d) Sare za michezo – Truck sut ya blue, Tshirt na Bukta ya blue zenye mistari meupe
e) Viatu vya Shule vyeusi vyenye visigino vifupi pamoja na viatu vya michezo.
f) Soksi jozi mbili (2) nyeupe
g) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
h) Sweeta rangi ya zambarau lenye nembo ya Shule, pia hupatikana Shuleni.
i) Tshirt ya kora rangi ya khaki yenye nembo ya Shule, pia hupatikana Shuleni.
j) Tai 2 rangi ya khaki zenye nembo ya Shule, pia hupatikana Shuleni.

**Tahadhari: Nguo za Nyumbani hazihitajiki, Mwanafunzi anaporipoti Shuleni anatakiwa kuvaa Suruali nyeusi na Shati nyeupe mikono mirefu.**

### 2:2. Mahitaji muhimu ambayo kila Mwanafunzi anapaswa kuja nayo:-

(i) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa na vyeti vya kitaaluma.
(ii) Ream 1 ya karatasi nyeupe “Double A” ( kwa kila muhula)
(iii) File 1 kwa ajili ya kutunzia taarifa za Mwanafunzi.
(iv) Vitabu vya masomo vya tahasusi husika
(v) Scientific calculator kwa Wanafunzi wa masomo ya Sayansi-FX 99 Original
(vi) Dictionary / Kamusi kwa Wanafunzi wa masomo ya lugha.
(vii) Madaftari 7 “Counter book quire 4”
(viii) Godoro kwa Mwanafunzi wa Bweni (Futi mbili na nusu).
(ix) Shuka 2 rangi ya blue, Blanketi 1, Mto wa kulalia 1 na Chandarua 1.
(x) Vyombo vya kulia chakula (Sahani, Bakuli, Kikombe na Kijiko)
(xi) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa ajili ya kutunzia maji na kuogea.
(xii) Kandambili pea moja kwa ajili ya kuogea na kuendea chooni.
(xiii) Taa ndogo ya solar kwa ajili ya dharua pindi umeme unapokatika.
(xiv) Sabuni ya chooni dumu la lita 5 kwa ajili ya kufanya usafi chooni na bafuni.
(xv)Sanduku la chuma (Trunker) 1, kwa ajili ya Mwanafunzi kutunzia vitu vyake.
(xvi) Kwanja 1, Jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

### 2:3. Viambatanisho muhimu vya kuja navyo kwenye fomu hii :-

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitari ya Serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi / Mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai
c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na taratibu za Shule.

## 3. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.

(i) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi, Wanafunzi wengine na jamii.
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kwa mujibu wa ratiba ya Shule.
(iii) Kushiriki kwa kila shughuli za Shule zitakazokuwepo.
(iv) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule
(v) Kuvaa sare za Shule wakati wote unapokuwa Shuleni.
(vi) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote.
(vii) Kutunza na kuzilinda mali za Shule.
(viii) Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation)
(ix) Kufahamu mipaka ya Shule na kuwa ndani ya Shule wakati wote.

## 4. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

(i) Kuwa nje ya Shule bila kibali cha Mwalimu wa zamu ama Mkuu wa Shule.
(ii) Kutovaa sare za Shule katika Mazingira ya Shule.
(iii) Wizi, udokozi, unyang'anyi na ujambazi.
(iv) Kutohudhulia masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
(v) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(vi) Kutoa lugha chafu kwa Wanafunzi wenzake, Walimu, Walezi na jamii.
(vii) Kupigana Mwanafunzi kwa Mwanafunzi ,kumpiga Mwalimu.
(viii) Kunyoa nywele kwa mitindo isiyo kubalika pamoja na kufuga ndevu
(ix) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(x) Uvutaji wa sigara, bangi na vilevi vingine.
(xi) Uasharati, uhusiano wa jinsia moja , kuoa au kuolewa.
(xii) Kumpachika mimba Mwanafunzi ama Mwanamke yeyote.
(xiii) Kushuriki matendo ya uhalifu na matendo yote yanayo vunja sheria za Shule
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na Nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xvi) Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(xviii) Uharibifu wa Mali za Shule na Umma kwa makusudi.

**NB: Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGUFULI**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ______________

**Jina la Mkuu wa Shule – ABDALLAH H. SESEME**

THE HEADMASTER
MAGUFULI HIGH SCHOOL
P. O. Box 76
C H A T O

# HALMASHAURI WILAYA YA CHATO

## SHULE YA SEKONDARI MAGUFULI

S . L . P - 7 6,

CHATO-GEITA

________________

### FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

MGANGA MKUU/MFAWIDHI,
KITUO CHA AFYA/HOSPITALI
……………………………………………
……………………………………………

YAH: KUJUA AFYA YA MWANAFUNZI KWA AJILI YA KUJIUNGA NA SHULE.

Kijana……………………………………………amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Magufuli.Naomba udhibitishe hali ya afya yake.Kabla hajaanza masomo rasmi hapa shuleni.

NB:Endapo atapatikana na tatizo lolote tunaomba utujulishe, na atakapopatikana na tatizo la kutoona vizuri, hana budi kujinunulia miwani kwa gharama zake mwenyewe.

Kwa Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Magufuli,
S . L . P – 7 6 ,
Chato-Geita .

YAH:AFYA YA ____________________________________________

Nimempima mtajwa hapo juu na kudhibitisha kuwa anasumbuliwa /hasumbuliwi na magonjwa yafuatayo

1) TB……………………………………………………………
2) HB……………………………………………………………
3) STOOL………………………………………………………
4) URINE………………………………………………………
5) EYE&EAR'S…………………………………………………
6) ATHMA………………………………………………………
7) THYPHOD……………………………………………………
8) OTHER

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

Maoni ya Daktari/Mganga mfawidhi……………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

JINA LA DAKTARI/MGANGA MFAWIDHI SAINI & MHURI

# HALMASHAURI WILAYA YA CHATO

## SHULE YA SEKONDARI MAGUFULI

## P.O.BOX–76 CHATO

**FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi.................................................Mwanafunzi wa kidato cha .......................mwaka.......................

Ninaahidi kwamba nitakuwa mwaminifu katika muda wangu wote wa masomo na katika kipindi chote nitakachokuwepo katika shule ya Sekondari Magufuli, kwa kutoshiriki katika Migomo, fujo na makosa ya jinai.

Pia naahidi kuwa nitakuwa mwaminifu kwa uongozi wa Shule na jumuiya nzima ya Shule ya Sekondari Magufuli, huku nikifuata sheria, taratibu na kanuni za shule kwa mujibu wa sheria za Wizara ya Elimu Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya ufundi.

Na pindi niendapo kijume na sheria na taratibu za shule, hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina la mwanafunzi .................................... sahihi................................tarehe........................................

Jina la mzazi/mlezi.......................................sahihi.................................tarehe...................................

Namba za simu za Mzazi/mlezi ........................,..........................................................................

# HALMASHAURI WILAYA YA CHATO

## SHULE YA SEKONDARI MAGUFULI

## P. O. B O X – 7 6  C H A T O

**<u>FOMU YA MKATABA KWA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA KULIPA MICHANGO YA SHULE PAMOJA NA MAELEKEKO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.</u>**

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Magufuli nakiri kukubaliana na Sheria, taratibu na kanuni za Shule.

Pia naahidi kutoa ushirikiana kwa Walimu na Uongozi wa Shule hususan katika swala zima la kulipa michango mbalimbali ya Shule pamoja na kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na uongozi wa Shule.

Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………………………sahihi……………………….tarehe…………………………

Namba za simu za Mzazi/Mlezi ……………………….,…………………………………………………………………………

# SHULE YA SEKONDARI MAGUFULI

## VIFAA VINAVYOPATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE NA GHARAMA ZAKE.

| S/N | MAHITAJI MUHIMU | GHARAMA ZAKE |
|---|---|---|
| 1 | Rimu "Double A" za karatasi nyeupe | 15,000/= |
| 2 | Spring file za kutunzia taarifa za Wanafunzi | 3,000/= |
| 3 | Scientific Calculator original "FX 99" | 60,000/= |
| 4 | Godoro Futi $2^{1/2}$ | 45,000/= |
| 5 | Sabuni ya chooni dumu la lita 5 | 10,000/= |
| 6 | Sanduku la Chuma "Trunker" | 30,000/= |
| 7 | Jembe lenye mpini | 7,000/= |
| 8 | Reki yenye mpini | 5,000/= |
| 9 | Fyekeo | 4,000/= |
| 10 | Mifagio ya ndani na nje. | 4,000/= |
| 11 | Ndoo ndogo yenye mfuniko. | 3,000/= |
| 12 | Daftari msomi | 800/= |
| 13 | Counter book Quire 4 | 4,500/= |
| 14 | Counter book Quire 3 | 3,500/= |
| 15 | Counter book Quire 2 | 2,500/= |
| 15 | Kandambili | 2,000/= |
| 16 | Chandarua | 5,000/= |
| 17 | Taa za solar | 10,000/= |